**MAADHIMISHO YA**

# SIKU YA POSTA AFRIKA

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

### TAMKO LA MSHESHIMIWA NAPE NNAUYE (MB), WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA POSTA AFRIKA (PAPU) TAREHE 18 JANUARI, 2022

Ninayo furaha kutoa tamko hili na salamu mahususi kwa Sekta ya Posta Afrika tunapoendelea kuadhimisha kuanzishwa kwa Umoja wa Posta Afrika (Pan African Postal Union - PAPU). Aidha, ninafurahi kuungana na Mawaziri wanaosimamia Sekta ya Posta katika Bara letu kutoa mchango katika kukuza Sekta hii muhimu. Kauli mbiu katika maadhimisho ya mwaka huu 2022 ni "Kuunganisha nguvu na wadau wa Posta Afrika".

Vilevile, ninafurahishwa kwamba Umoja wa Posta Afrika umeendelea kuwa mshirika kwa Serikali katika kukidhi malengo ya nchi za Afrika. Mashirika ya Posta yamekuwa ni chombo kinachoaminika kwa kusafirisha na kubadilishana nyaraka na vifurushi kwa miaka mingi katika historia. Huduma za posta zinaendelea kuwa za muhimu wakati wa sasa kwa kusambaza maarifa na habari; kuchangia utoaji elimu kwa kupitia mtandao; kuwezesha biashara; kuchangia katika utafiti, ubunifu na maendeleo. Sekta hii ina mchango muhimu katika kutekeleza malengo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, **Mh. Nape Nnauye (Mb).**

Watoa Huduma za posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto, wakiwa ni watoa Huduma duniani kote, wanawezesha urahisi, usalama na gharama nafuu za usafirishaji wa bidhaa na rasilimali katika mnyororo wa thamani. Maendeleo na matumizi ya TEHAMA katika miaka ya karibuni, yamewezesha ubunifu katika kuendesha biashara mtandao ambayo inatoa fursa kwa mapato mapya katika kutengeneza utajiri hasa kwa ukuaji wake wa kasi. Watoa Huduma hawa wamebadili kabisa michakato ya biashara zao na viwango vya utendaji ili kwenda sambamba na ukuaji wa teknolojia.

Uwezeshaji unaoletwa na maendeleo ya teknolojia umeifanya Tanzania kuwa kati ya nchi zinazoongoza barani Afrika katika kutumia teknolojia katika utoaji huduma za posta ambazo zinajumuisha utumiaji wa TEHAMA katika kaunta zake, mfumo wa ufuatiliaji katika mnyororo wa thamani, barua za kieletroniki, utumaji fedha kwa njia za kieletroniki na kupima ubora wa huduma zake kwa mfumo wa utambuzi wa kisasa. Inategemewa kwamba matumizi kamili ya TEHAMA katika Posta itawezesha utoaji wa huduma zinazohitajika za kuaminika, nafuu na zenye ubora wenye kukolezwa na teknolojia. Barua za kieletroniki ambazo ni mchanganyiko usafirishaji wa kieletroniki na ufikishwaji wa nyaraka na mizigo na huduma zingine kadhaa za kimtandao zenye kubebwa na intaneti ni mifano ambayo inaweza kutolewa kuboresha huduma za posta.

Kauli-mbiu ya mwaka huu "Kuunganisha nguvu na wadau wa Posta Afrika'' inatokana na mjadala wa kuufungua Umoja wa Posta Duniani uliofanyika katika Mkutano Mkuu wa 27 Jijini Abidjan, Ivory Coast, mwezi Agosti, 2021. Ilikubaliwa kuwa ufunguaji wa Sekta ya Posta kuwahusisha wadau wengine iambatane na mageuzi kwenye Sekta ambayo yana uwanda mpana kuhusisha uondoaji wa vikwazo vya biashara, ubinafishaji na kuongezeka kwa biashara mtandao. Ni muhimu kufahamu kwamba watoa huduma wa wengine ni Mamlaka ya Mapato na Ushuru wa Forodha, watoa Huduma kwa Mashirika ya Posta na waliomo kwenye mnyororo wa thamani wa shughuli za posta. Katika mjadala ule ilijadiliwa kuwa manufaa makubwa kwa kuifungua Sekta ya Posta ni pamoja na kuimarisha utoaji wa huduma na kuchagiza maendeleo ya biashara mtandao.

Sote tunatambua kuwa utumaji wa barua umebebwa na mawasiliano ya kieletroniki, wakati huu biashara mtandao imeongezeka sana kwa utumaji na ufikishaji wa vifurushi na vipeto. Ushirikiano wa wadau ni kitu muhimu katika kudhibiti miundombinu ya posta kwa Bara la Afrika. Katika miaka ya hivi karibuni, Mamlaka za udhibiti zilijikita zaidi katika udhibiti kwenye utumaji wa barua; mageuzi ya kidijitali na ukuaji wa biashara mtandao na kufanya mtazamo wa watoa Huduma za posta katika nchi zetu kujikita katika biashara za vifurushi, vipeto, mizigo na bidhaa. Matumizi ya viwango pamoja na teknolojia vimeongeza usahihi na uhakika wa kisheria na kuwezesha kupunguza gharama na masuala ya muingiliano ya utendaji. Kazi hii ni ya wadhibiti wa Sekta ya Posta na tunahitaji kuimarisha na kuiweka sawia miundo ya udhibiti Barani Afrika.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, imedhamiria kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya uendeshaji wenye ufanisi wa Sekta ya Posta. Kwa kuzingatia hayo, Sera ya Taifa ya Posta iliyohuishwa itaweka matamko yatakayowezesha utekelezaji wa kaulimbiu ya maadhimisho haya ya Siku ya Posta Afrika. Wizara ninayoiongoza yenye dhamana ya teknolojia, tutaimarisha programu za elimu kwa umma nchi nzima, ili watoa Huduma za posta na wadau wengine watumie kikamilifu TEHAMA katika utoaji wa Huduma. Kwa muktadha huu, huduma za posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto zitaendelea kuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa Tanzania na jamii ya habari. Ninaamini kwamba miundombinu ya posta utaendelea kubaki kuwa yenye faida na njia ya uhakika ya kubadilishana habari kwa muda mrefu ujao.

Ninatazamia Sekta ya Posta ya Afrika yenye mafanikio kwa siku zijazo.

**Heri ya Mwaka Mpya 2022**
**KAZI IENDELEE**
**Ninawashukuru sana.**

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI
## MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)

### UJUMBE WA MKURUGENZI MKUU WA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA), DKT. JABIRI K. BAKARI KWENYE MAADHIMISHO YA 42 YA UMOJA WA POSTA AFRIKA – PAN AFRICAN POSTAL UNION (PAPU) TAREHE 18 JANUARI 2022

Kwa furaha kubwa, Tanzania inaungana na nchi nyingine Barani Afrika wanachama wa Umoja wa Posta Afrika (PAPU) kuadhimisha miaka 42 ya kuasisiwa kwa umoja huu. Leo ni Siku ya Posta Afrika. Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ninapenda kuipongeza PAPU na sekretarieti yenye makao makuu Arusha, Tanzania kwa maadhimisho ya siku hii muhimu.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), **Dkt. Jabiri K. Bakari.**

Kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ni "Kuunganisha nguvu na wadau wa Posta Afrika".

Mchakato wa kuboresha sekta ya posta barani Afrika unahitaji majadiliano endelevu, ushirikiano, kujenga imani na kubadilishana ujuzi na uzoefu miongoni mwa wanachama. Kufanya kazi pamoja badala ya kuendeleza mashindano yasiyo na tija ni njia muhimu na ya kipekee inayoweza kuipa uhai mijadala hii.

Kwa kuunganisha nguvu za wadau wote katika sekta ya Posta, ukuzaji wa uchumi wa kidijitali na maendeleo ya haraka yanayoshuhudiwa katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) vinatoa fursa ya kipekee katika kukuza sekta ya posta Afrika. Suala hili litawezekana kupitia ushirikishwaji wa wadau wote. Tukizingatia kwamba ubunifu siyo suala la kuchagua, bali lazima; sekta ya posta katika mazingira hayo inalazimika kuongeza jitihada katika kushirikiana na wadau mbalimbali hasa wadau wa nje. Ili kufanikiwa katika shughuli zake, inapotekeleza mipango ya kuleta mabadiliko, ni muhimu sekta ya Posta kuzingatia ubia kati ya sekta binafsi yaani public-private partnerships (PPP) kama njia muhimu ya kukusanya nguvu na kufanya kazi na wadau wengine huku ikipima matokeo, faida na hasara za hatua hizo. Aidha uchanganuzi wa mifumo ya kisheria na ki-udhibiti kwa kazi husika katika sekta, ni muhimu; na unapaswa ufanywe kwa kuzingatia mazingira na hali ya soko.

Ni muhimu na izingatiwe kwamba, wasimamizi wa sekta ya posta barani Afrika wanapaswa kufuata mpango-mkakati uliomakinika, wafanye uchanganuzi wa masuala mtambuka ya kisekta, waunde na kusimamia mpango-mkakati na kutafuta suluhisho bora zaidi linalowezesha miradi yao mahusus kufanikiwa.

Janga la UVIKO-19 linaloikabili dunia hivi sasa linaonyesha uzito na haja ya sekta ya Posta kufanya kazi na wadau wengine wa sekta hiyo katika kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi; kwa kuzingatia ukweli kwamba huduma za Posta katika zama za sasa zinatumia TEHAMA kuboresha michakato ya biashara na kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya wateja wenye ujuzi wa kidijitali - ili kuhakikisha wanaendelea kunufaika kiuchumi, kibiashara, na kijamii sasa na katika siku zijazo; hivyo katika muktadha

# MAADHIMISHO YA
# SIKU YA POSTA AFRIKA

huu ni lazima posta ifanye kazi na wahusika wengine wa sekta.

Katika kipindi hiki ambacho dunia inapambana na UVIKO-19 ni muhimu kwa Posta kushirikiana na wadau wengine wa sekta katika kutoa huduma kwa jamii. Kuenea kwa janga la UVIKO-19 na kubadilika kwa mazingira ya kufanyia kazi kumebadili namna ambavyo tunaishi, kuendesha shughuli zetu za kila siku na kutumia huduma. Kwa hali hii, kwa kuunganisha nguvu na washirika wengine wa sekta ya Posta tunatakiwa kuhakikisha Posta inakuwa sehemu ya suluhisho wakati huu dunia ikipitia wakati wa changamoto ya UVIKO-19.

Ubia katika utoaji wa huduma kipindi hiki cha changamoto umechangia katika kuwawezesha wateja wa sekta ya Posta kuhamia kwa haraka mitandaoni.

Mawasiliano ya kidijitali yanazisukuma huduma za posta kupewa msukumo mpya na kupambanua ubunifu mpya katika kufikisha huduma kwa mtumiaji mwisho, hasa kwa huduma za biashara-mtandao. Kwa hiyo, ipo haja ya kuhimiza umuhimu wa kuongezwa ufanisi katika utoaji wa huduma za posta za kidijitali.

Kama njia ya kuunganisha nguvu za washiriki wa sekta pana ya Posta, TCRA kwa kushirikiana na watoa huduma za Posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto, inapitia upya miongozo ya sekta kwa kuweka viwango vipya vya utoaji huduma, sehemu za kufikisha huduma na vipindi vya kufikisha bidhaa zinazotumwa, ili kutatua changamoto zinazochagizwa na janga la UVIKO-19.

Wanachama wa PAPU wanatakiwa kuendelea kutimiza wajibu wao muhimu katika kujenga eneo moja la Posta Afrika wakati wote na katika mazingira yote kwa kuchangia juhudi zao katika kutekeleza azma ya pamoja ya watu wa Afrika kuwa na Maendeleo jumuishi na endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Ili kuhakikisha nchi za Afrika zinaweka mipango ya kuchangia nguvu za washiriki wa sekta pana na Posta, Tanzania, kupitia TCRA imeazimia na inategemea kuona jengo la Makao Makuu ya PAPU, litakalojulikana kama PAPU House linakamilika kwa wakati ili kuonyesha kwa vitendo mafanikio ya juhudi zilizofanyika katika miongo minne iliyopita kuinua jengo hilo la ghofofa 18 ambalo litapamba anga za jiji la Arusha. Kuunganisha vyema nguvu za washiriki kutaiwezesha Afrika kujenga taasisi zenye nguvu; sasa na baadae, katika kuelekeza Afrika kwenye maendeleo yanayohitajika kwa ustawi wa watu wake.

Katika kufanikisha uchangiaji wa nguvu na washiriki wa sekta ya Posta Afrika, TCRA itaendelea kushirikiana na PAPU katika maeneo yote yanayohusiana na ujenzi wa sekta imara ya posta. Vilevile, katika kushirikisha washiriki wengine wa sekta imeweka mfumo mzuri wa leseni ili kwamba viwango vya huduma vinaboreshwa kwa wateja wengi. Tunatarajia kwamba wateja wa posta wataendelea kufaidi huduma mbalimbali za posta za uhakika, zenye ubunifu na zinazomjali mteja.

Hadi leo, TCRA imetoa leseni kwa watoa huduma 135 wa posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto, ambao wako kwenye makundi sita tofauti kama inavyoonekana kwenye jedwali.

**Jedwali: Aina ya huduma na leseni zilizotolewa**

| Na | Aina ya Leseni | Jumla |
|---|---|---|
| 1. | Mtoa huduma za Posta | 1 |
| 2. | Wasafirishaji wa vifurushi na vipeto kimataifa | 5 |
| 3. | Wasafirishaji wa vifurushi na vipeto Afrika Mashariki | 1 |
| 4. | Wasafirishaji wa vifurushi na vipeto nchini | 35 |
| 5. | Wasafirishaji wa vifurushi na vipeto ndani ya miji | 23 |
| 6. | Wasafirishaji wa vifurushi na vipetokati ya miji | 6 |
| 7. | Watoa huduma za usafiri wanaosafirisha vifurushi na vipeto kati ya miji | 64 |
| | **JUMLA** | **135** |

TCRA itaendelea kusimamia sekta ya posta kwa ufanisi ili kufanikisha na kuwawezesha wateja wa posta kufaidika kikamilifu kutokana na mabadiliko ya kijamii, kiteknolojia na kiuchumi.

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya TCRA, Menejimenti na Watumishi, ninapenda kuwapa wadau wa sekta ya Posta salamu za Heri ya Mwaka 2022 na kuwatakia mafanikio wanapotumia huduma za mawasiliano ya posta.

**Asanteni sana.**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI
# SHIRIKA LA POSTA TANZANIA

**UJUMBE WA POSTAMASTA MKUU KWENYE MAADHIMISHO YA SIKU YA UMOJA WA POSTA AFRIKA (PAPU) TAREHE 18 JANUARI, 2022**

***KAULI MBIU: "Kuunganisha nguvu na wadau wa Posta Afrika"***



**Kaimu Postamasta Mkuu**
**Macrice Daniel Mbodo**

Leo tarehe 18 Januari, 2022 tunapoadhimisha siku ya Posta Afrika , tunaelewa kuwa dunia yetu imepitia wakati mgumu tangu 2019 hadi 2021 kwa sababu ya janga la UVIKO-19, janga hili limebadilisha kabisa maisha na namna ya kufanya mambo, janga hili limechukua maisha ya watu wengi duniani na kusababisha biashara kuyumba,- makampuni mengi yamefungwa na mengine kupunguza shughuli zake, Uchumi umeshuka kwa kiwango kikubwa sana. Hata hivyo tunakubali kuwa siyo sekta ya posta pekee Afrika bali ni duniani kote imetikiswa na janga hili iwe ni moja kwa moja au kwa kupitia shughuli wafanyazo. Pamoja na haya yote tunashukuru Posta imejipambanua kwa kuendelea kuwepo na kutoa huduma hata katikati ya janga hili.

Tunapoadhimisha siku hii muhimu ya Umoja wetu wa PAPU, nitumie fursa hii kuwapongeza Katibu Mkuu wa PAPU Bwana Sifundo Chief Moyo na Katibu Mkuu Msaidizi Bibi Jessica Hope Ssengooba kwa kuaminiwa na nchi wanachama na kuwachagua kuongoza kwa kipindi cha miaka minne 2022-2025. Kwa kuwa maadhimisho haya ni ya mara ya kwanza kwenu mkiwa ofisini, niwatakie kila la heri na imani mliyopewa na wanachama muitendee haki ili kuendeleza Sekta ya mawasiliano ya posta barani Afrika. Shirika la Posta Tanzania likiwa ndiye mteule wa Serikali wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mwenyeji wenu katika masuala ya posta hapa nchini, niwahakikishie ushirikiano wetu uliotukuka kwenye majukumu yenu haya kuendeleza sekta ya Posta Barani Afrika.

Serikali nyingi duniani zilifunga mipaka na kuweka vizuizi vya safari ili kuzuia kuenea kwa janga hili. Zaidi ya asilimia 80% ya bidhaa zilipatikana kupitia biashara mtandao ambao posta pia ni mshirika kwenye biashara mtandao na uwezeshaji wake. Ukuaji wake unahitaji mipango thabiti kwenye mpangilio wa kufuatilia ukuaji wa teknolojia na hii ndiyo inayotufanya sisi kama Posta kufanya mageuzi makubwa ili kuendana na maendeleo haya ili kutuwezesha kutimiza wajibu wetu.

Katika kutafuta suluhisho la usimamizi wa mfumo wa posta katika mnyororo wa ugavi, mabadiliko kadhaa ya mfumo ili kukuza ubadilishanaji wa data za kielektroniki na waendeshaji Wateule wa Posta kupitia ubadilishanaji wa data wa kielektroniki wa Umoja wa Posta Duniani (UPU-EDI) yamefanywa ili kuruhusu wadau zaidi kusaidia kuibua na kutatua hitilafu katika mnyororo wa usambazaji wa posta. Upatikanaji wa suluhu katika mnyororo wa ugavi huunganisha wadau wengine kama vile forodha, watoa huduma za usafiri wa ndege na njia nyinginezo za usafiri kama vile kampuni za baharini, barabara na reli, hizi zina athari ya moja kwa moja katika mfumo wa usimamizi wa ugavi mtandaoni unaotumiwa na watoa huduma za posta wateule.

Kwa msingi huu, tunakubaliana na msemo wa wahenga wa kiafrika waliosema "ukitaka kwenda haraka nenda peke yako, lakini ukitaka kwenda mbali zaidi nenda na wenzako" hii inamaanisha tukifanya pamoja wote tunanufaika zaidi. Posta ni Sekta inayohusu jamii, tunapofanya mageuzi kwenda kidijitali tunaichukua jamii nzima, tunawashirikisha wengine katika jamii na wadau ili kupata manufaa ya pamoja. Tumejidhatiti kwa hali zote kuzingatia mabadiliko ya teknolojia , kuwa na mifumo mipya ya kibiashara inayokidhi mahitaji ya wateja, tunafika mbali zaidi kwa kuzingatia ubunifu kuwa ndiyo msingi endelevu wa utoaji huduma kwa wananchi wetu huku tukiwashirikisha wadau wengine.

Safari ya mageuzi TPC inayoendelea inahusisha washirika wa sekta mbalimbali ambao hushirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na mabenki, makampuni ya bima, wanambari na taasisi ya teknolojia nchini Tanzania. Haya yote yana nafasi tofauti katika shughuli zetu. Mabenki hurahisisha malipo kwa wakati mmoja, sisi hufanya kazi kama mawakala wao na hivyo umma kuvutiwa na ofisi za posta kuja kupata huduma zingine, huduma za bima halikadhalika nao hutoa huduma ndani ya majengo yetu na vyombo vya habari vinao umuhimu huo, ikiwa tutafanya juhudi zote za mageuzi na chochote tunachoweza kutoa jamii yetu na hakuna anayefahamu tunachofanya hizi zote zitakuwa ni juhudi za zisizo na faida kama wananchi wetu hawajui, hapa ndiyo tunapohitaji wanahabari kupeleka taarifa hizi kwa umma.

Tunayo safari ya mageuzi kwa hiyo tunafanya ubunifu siku baada ya siku na tunatumia teknolojia ya kuwezesha kufanya kile tunachotaka kutoa kwa umma wa Watanzania,kwa hivyo tunakuja na wazo jipya washirika wetu katika Taasisi ya Teknolojia wanatusaidia kuleta suluhisho kwa kushirikiana na wataalam wetu wa ndani wa TEHAMA.

Tunayo mifumo ambayo tunaitumia kwa sasa ikiwa ni matunda ya wataalam wetu wa ndani.

Maendeleo ya uchumi wa kidijitali hayawezi kubebwa na mtu au watu wachache, zinahitajika juhudi za makusudi za pamoja na hii inategemea wadau mbalimbali kama inavyosema Kaulimbiu ya maadhimisho ya PAPU ya mwaka huu. Katika kutoa huduma za za kidijitali za hatutaraji kuzifanya peke yetu bila wadau wetu kama tulivyoeleza hapo mwanzo, huduma za posta zinalenga kukuza uchumi jamii na hivyo hatutaacha mtu nje ya wigo wa huduma zetu. Hii ina maana tunazingatia tamko la Umoja wa Mataifa kuwa kila mwananchi anayo haki ya kupata huduma za mawasiliano ya posta popote alipo bila kujali gharama za kufikisha hapo, hii ni kuzingatia (Huduma Jumuishi kwa Wote-USO).

Tunapoendelea mbele katika kuimarisha ushirikiano na wadau zaidi wa sekta ya posta, tumejipanga kikamilifu kuwahudumia watu wote kwenye jamii zetu huku tukizingatia maslahi ya kila mshirika wetu, kwetu Shirika la Posta tupo tayari kwa ushirikiano wenye faida na tunatambua hukuna anayeweza kufanya peke yake. Tunawakaribisha wadau zaidi kutumia fursa ya mtandao wetu mpana kabisa nchini , mtandao wenye muunganiko na Afrika na Dunia yote ili waweze kuwafikia wananchi wengi popote walipo huku tukizingatia mahitaji yao.Hii inalenga kuwapa wananchi wanachokihitaji.

Siku ya leo tunaposherehekea siku ya PAPU, nitumie fursa hii kuwashukuru wateja wetu wapendwa, Wadau, Serikali na Umma wa Watanzania kwa kutuamini na kutuunga mkono katika mwaka wote wa 2021, hivyo kutufanya vinara wa utoaji huduma kwenye soko la posta nchini.

Naomba nihitimishe ujumbe wangu kwenu wateja, wadau wote na umma kwa ujumla kuwatakia Heri ya Mwaka mpya 2022 na natarajia tutaendelea kushimana pamoja

**Pamoja tunajenga Sekta ya Posta**
**Pamoja tunajenga Taifa letu,**
**Pamoja tunajenga bara letu Afrika!**
**Nawashukuru sana**

**Macrice Daniel Mbodo**
**Kaimu Postamasta Mkuu.**